



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA



(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu; 0232935443

Nukushi; 0232935442

Baruapepe: td@nanyambatc.go.tz

2 BARABARA YA BOMAN

S.L.P 1490,

63682 NANYAMBA-MTWARA

Tarehe: 05/10/2022

TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA ANAWATANGAZIA WAKAZI WOTE WA HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA KUWA ANATOA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU. FEDHA HIZI ZA MIKOPO ZINAZOTOKANA NA ASILIMIA 10 YA MAKUSANYO YA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI NA MAREJESHO YA MIKOPO ILIYOKOPESHWA KWENYE VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 HALMASHAURI INATARAJIA KUKUSANYA NA KUTENGA KIASI CHA SHILINGI **214,096,650.00 (TSHS. 130,846,650.00 ZA ASILIMIA KUMI NA TSHS.83,250,000.00 ZA MAREJESHO)** KWA WANAWAKE IMETENGWA KIASI CHA SHILINGI **85,638,660.00** VIJANA KIASI CHA SHILINGI **85,638,660** NA WATU WENYE ULEMAVU KIASI CHA SHILINGI **42,819,330** KWA UWIANO WA *ASILIMIA 4 WANAWAKE/ASILIMIA 4 VIJANA/ASILIMIA 2 WATU WENYE ULEMAVU.*


TARATIBU ZA UOMBAJI WA MIKOPO

1. WANANCHI WANATAKIWA KUJIUNGA KWENYE VIKUNDI VYA WATU WATANO HADI KUMI NA KUSAJILIWA. KWA KUNDI LA WATU WENYE ULEMAVU WATU WAWILI HADI WATANO NA PALE KWENYE KIJIKI/MTAA MTU MWENYE ULEMAVU ANAKUWA MMOJA HUYU ANAWEZA KUOMBA MIKOPO YEYE PEKEYAKE.
2. KIKUNDI KINATAKIWA KIANDIKE BARUA YA MAOMBI YA MIKOPO NA KIJAZE FOMU MAALUMU INAYOTOLEWA NA HALMASHAURI YA MJI KUPITIA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII NA KATIKA OFISI ZA WATENDAJI WA KATA
3. BARUA YA MAOMBI YA MIKOPO PAMOJA NA FOMU MAALUMU IJAZWE KIKAMILIFU NA KUAMBATANISHWA NA NAKALA HALISI ZA NYARAKA ZIFUATAZO
❖ KATIBA YA KIKUNDI

- ❖ CHETI CHA UTAMBUZI/USAJILI WA KIKUNDI
- ❖ LESENI YA BIASHARA/ VITAMBULISHO VYA UJASILIAMALI
- ❖ TAARIFA KUTOKA KWA MTENDAJI WA KIJIKI/ KATA KUWA ANAWATAMBUA
- ❖ ANDIKO LA MRADI WA KIKUNDI/ MPANGO WA BIASHARA
- ❖ KWA MTU MWENYE ULEMAVU ANAYEOMBA MKOPO MTU MMOJA, AWASILISHE BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA KWA MTENDAJI WA KATA/KIJIKI INAYOMSHUHUDIA KUWA AMEKOSA WENZAKE WENYE ULEMAVU WA KUJIUNGA NAO KWENYE KIKUNDI
- ❖ VITAMBULISHO VYA NIDA KWA WANACHAMA WOTE NI LAZIMA.
- ❖ PICHA (PASSPORT SIZE) ZA WANACHAMA WOTE WA KIKUNDI
- ❖ MUHTASARI WA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA (WDC) ULIOPIITISHWA NA MTENDAJI WA KATA JUU YA KIKUNDI KUPEWA MKOPO UAMBATANISHWE.
- ❖ KWA VIKUNDI VYA VIJANA WANACHAMA WANATAKIWA WAVE NA UMRI WA MIAKA 15 HADI 35.
- ❖ MAOMBI YA MKOPO YATAFANYWA KWA NJIA YA MFUMO WA USIMAMIZI NA UTOAJI WA MIKOPO (TPLMIS) HIVYO NI VYEMA WANACHAMA KUPIKA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII KWA AJILI YA MAELEKEZO YA KUTUMIA MFUMO HUO.

BARUA YA MAOMBI, VIAMBATANISHO NA FOMU MAALUM ILIYOJAZWA KIKAMILIFU ZITUMWE/ZIWASILISHWE OFISI YA MTENDAJI WA KATA KWA KUPITISHWA NA KUPELEKWA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA

NB: WANANCHI WENYE AJIRA RASMI HAWARUHUSIWI KUOMBA MIKOPO HII KWA MUJIBU WA MWONGOZO WA KANUNI ZA UTOAJI WA MIKOPO HII.



Thomas E. Mwilafu
**MKURUGENZI WA MJI
 NANYAMBA**

